


## UTABIRI WA MVUA ZA VULI (OKTOBA – DISEMBA, 2020) KWA WILAYA YA KASKAZINI “B”, UNGUJA

Umetolewa: 08/09/2020

Taarifa hii inatoa mwelekeo wa msimu wa mvua za *Vuli* katika kipindi cha Oktoba – Disemba, 2020 na athari zake kwa sekta za kilimo, mifugo na uvuvi katika Wilaya ya Kaskazini “B”, Unguja.



### Mvua za Msimu wa Vuli (2020) kwa Wilaya ya Kaskazini “B”

**Zitaanza:** Wiki ya nne ya mwezi Oktoba, 2020.

**Zitaisha:** Mwezi Januari, 2021.

**Urefu wa Msimu wa Mvua:** Kijumla unatarajiwa kuwa mfupi.

**Kiasi cha mvua zinazotarajiwa:** Wastani hadi chini ya wastani

**Kiwango cha juu cha mvua:** Kinatarajiwa katika miezi ya Oktoba na Novemba, 2020.

**Vipindi vya ukavu:** Upo uwezekano wa kutokea vipindi vifupi vya ukavu kati ya wiki ya tatu na nne ya mwezi Disemba, 2020.

**Mtawanyiko:** Mvua zinatarajiwa kuwa na mtawanyiko wa kuridhisha katika maeneo mengi.

#### Angalizo:

- Watumiaji wa taarifa hii wanashauriwa kufuatilia utabiri wa siku 10, saa 24 pamoja na tahadhari kila zinapotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania.
- Wakulima, wafugaji na wavuvi wanashauriwa kupata ushauri zaidi kutoka kwa maafisa ugani kwa matumizi sahihi ya taarifa za utabiri wa hali ya hewa.

### Matokeo na ushauri kwa kilimo, mifugo na uvuvi

#### Matokeo

- Unyevunyevu ardhini unatarajiwa kuwa wa kuridhisha katika maeneo mengi hususan magharibi mwa wilaya Kaskazini B.
- Maji na malisho ya wastani kwa ajili ya mifugo yanatarajiwa, hata hivyo uwezekano wa upungufu kidogo kwa ukanda wa Mashariki unatarajiwa.
- Magonjwa ya mifugo, na wadudu waharibifu wa mazao yanaweza kujitokeza.
- Upatikanaji wa mazao ya baharini (samaki na mwani) unatarajiwa kuwa wa kawaida.

#### Ushauri

- Wakulima kutumia mbegu bora zinakomaa mapema na kustahmili magonjwa mfano viazi vitamu, kunde na mihogo kamavile, Kizimbani, Machui, kama na Mahonda.
- Wafugaji wanashauriwa kuhifadhi chakula kwa ajili ya mifugo ili kukabiliana na upungufu unaoweza kujitokeza.

Utabori wa hali ya hewa nchini na tahadhari zinapatikana katika tovuti ya Mamlaka: [www.meteo.go.tz](http://www.meteo.go.tz)

Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:

Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Morogoro Rd, Ubungo Plaza, Ghorofa ya 3, S.L.P. 3056, Dar es Salaam, Tanzania. Nukushi: +255 22 2460735, Simu: +255 22 2460706-8.

Barua pepe: [met@meteo.go.tz](mailto:met@meteo.go.tz), Tovuti: [www.meteo.go.tz](http://www.meteo.go.tz)

(IMETHIBITISHWA – ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)

105A – 09/19